

# HUDUMA ZA MLIMA WA MOTO NA MIUJIZA

Makao Makuu ya Kimataifa, Lagos, Nigeria.

2022 UKOMBOZI WA WANAWAKE.

Maagizo

- Tumia dakika chache wa kumsifu Bwana.
- Ungama dhambi unazozijuwa kwa Bwana.
- Muombe Bwana alete kwenye kumbukumbu zako sehemu au milango lliyofunguliwa ambayo nguvu za kiroho za uovu zinaweza kutumia kuingia kwenye maisha yako.
- Ingia kwenye kipindi hiki cha maombi ya ukali. Vipengele vyote vya Maombi vinafanywa kwa hasira za Rohoni, vurugu na kwa fujo iliyoamuliwa.

Kukiri: **Wagalatia 3:13-14:** Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu; maana imeandikwa, Amelaaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti;

ili kwamba baraka ya Ibrahimu iwafikilie Mataifa katika Yesu Kristo, tupate kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya imani.

**Isaya 54:17:** Kila silaha itakayofanyika juu yako haitafanikiwa na kila ulimi utakaoinuka juu yako katika hukumu utauhukumu kuwa mkosa. Huu ndio urithi wa watumishi wa Bwana, na haki yao inayotoka kwangu mimi, asema Bwana.

**Ufunuo 12:11:** Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa.

1. Mshukuru Bwana kwa nguvu ilioko katika damu Yesu ambayo haiwezi kushindwa.
2. Bwana, tembea nyuma kwenye mti wa familia yangu na ufanye nguvu yako ya Uponyaji udhihirike.
3. Ninajiachilia ,Kwa Jina la Yesu, kutoka kwa Kila laana ya ndoa na ukoo.
4. Ninakataa na kuvunja laana zote na uchawi uliowekwa juu ya maisha yangu ya ndoa, Kwa Jina la Yesu.
5. Ninachukua mamlaka juu na kufunga kila mtu mwenye nguvu kwenye sehemu yoyote ya maisha yangu.

6. Kwa Jina la Yesu, Ninavunja laana zote za ndoa zilizowekwa juu yangu na maadui za nyumbani kwangu.
7. Chochote ambacho kilicho ndani yangu ambacho ni kinyume cha ndoa kiasili, ondoka sasa, Katika Jina la Yesu.
8. Kila muundo wa uovu katika familia kinyume cha ndoa, vunjika, Kwa Jina la Yesu.
9. Ninakataa, vifungo vya uovu vya nafsi vinavyo jificha, Katika Jina la Yesu.
10. Acha mfalme wa amani atawale kwenye ndoa yangu bila kizuizi, Katika Jina la Yesu.
11. Nguvu zote zinazofanya njama na yeyote kuharibu nyumba\ndoa yangu, achia, Katika Jina la Yesu.
12. Acha kila nguvu inayotaribu kuchora mpya ramani ya ndoa yangu, ihaibike, Katika Jina la Yesu.
13. Ee Bwana, fanya familia yangu kuwa tangazo la nguvu yako, Katika Jina la Yesu Kristo
14. Najiachilia kutoka kwa kila uchafuzi wa ndoto, Katika Jina la Yesu.
15. Acha vifaa vyote hasi vinavyozunguka kwenye mtiririko wa Damu yangu, viondolewe, Katika Jina la Yesu.
16. Moto wa Roho Mtakatifu, Safisha maisha yangu.
17. Ving'ora vya Kichawi, vinavyolia kutoka kwenye msingi wangu ili kufukuza wasaidizi wangu, kufa, Katika Jina la Yesu.
18. Bahati mbaya, Kiti cha nyuma, maisha ya msukosuko, iliyonenwa kwenye maisha yangu, haribika, Katika Jina la Yesu.
19. Weka mkono wako moja juu ya kichwa chako na ingine kwenye tumbo lako au sehemu ya kitovu na uanze kuomba hivi;  
Moto wa Roho Mtakatifu waka kutoka utosi wa kichwa hadi nyayo za miguu. Anza kutaja kila kiungo cha mwili wako; figo yako, ini, utumbo, damu n.k. Usiwe na haraka kwenye sehemu hii, kwasababu hakika moto utakuja na utaanza kuhisi joto.
20. Mshukuru Bwana kwa Kujibu Maombi yako.